**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 5, Issue 1, 2022**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Uamilifu wa Kipragmatiki wa Kirai Nomino (KN) Katika Kiswahili

*Chege Joel Ngari*[1*]

[1] Chuo Kikuu cha Kenyatta, S. L. P. 43844-00100, Nairobi, Kenya.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0000-0002-9630-3932; Barua pepe ya mawasiliano: joelchege867@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.853**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*21 Septemba 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*Kishazi, Muundo, Muktadha, Kirai, Kiima, Ufasili, Pragmatiki.*

## IKISIRI

Makala haya yalitalii uamilifu wa kipragmatiki wa kirai nomino katika sintaksia ya Kiswahili. Pragmatiki hujihusisha na namna watu wanavyotumia lugha katika muktadha na hali halisi ya mawasiliano. Hivyo basi, pragmatiki ni taaluma inayochunguza maana kulingana na muktadha fulani. Miongoni mwa maana za kimuktadha zilizoshughulikiwa ni pamoja na: maana dhanishi, maana tagusanishi na maana matinishi. Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni Sarufi Amilifu Mfumo (SAM) iliyopendekezwa na Halliday. Umuhimu wake ni kwamba inaeleza jinsi lugha inavyotumika katika hali halisi ya mawasiliano. Mbinu za utafiti zilizoongoza utafiti huu ni mahojiano na uchunzaji. Mbinu ya uchunzaji ilitumika ambapo maongezi ya wazungumzaji yalirekodiwa. Mbinu hizi zilikamilishana na kujengana kila mojawazo ikisawazisha mapungufu ya nyingine. Data ya maktabani ilitumika kuweka misingi ya ukusanyaji wa data ya nyanjani ambayo ilikusanywa kwa maswali ya mahojiano. Data katika makala haya ilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya majedwali na maelezo. Walengwa wa utafiti huu walikuwa ni: wahadhiri na walimu, vijana waliomaliza shule ya upili na vyuo na wanafunzi wa shule za upili na vyuo. Makala haya yaliweka bayana namna kirai nomino kinavyoweza kutumika kufumba ujumbe kipragmatiki katika mawasiliano. Makala haya yanatoa nafasi ya kupigiwa mfano ya kuchangia katika taaluma ya pragmatiki na isimu kwa jumla.

**APA CITATION**

Ngari, C. J. (2022). Uamilifu wa Kipragmatiki wa Kirai Nomino (KN) Katika Kiswahili. *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(1), 330-340. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.853.

**CHICAGO CITATION**

Ngari, Chege Joel. 2022. "Uamilifu wa Kipragmatiki wa Kirai Nomino (KN) Katika Kiswahili". *East African Journal of Swahili Studies* 5 (1), 330-340. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.853.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.853

**HARVARD CITATION**
Ngari, C. J. (2022) “Uamilifu wa Kipragmatiki wa Kirai Nomino (KN) Katika Kiswahili”, *East African Journal of Swahili Studies*, 5(1), pp. 330-340. doi: 10.37284/jammk.5.1.853.

**IEEE CITATION**
C. J. Ngari, “Uamilifu wa Kipragmatiki wa Kirai Nomino (KN) Katika Kiswahili”, *EAJSS*, vol. 5, no. 1, pp. 330-340, Sep. 2022.

**MLA CITATION**
Ngari, Chege Joel. “Uamilifu wa Kipragmatiki wa Kirai Nomino (KN) Katika Kiswahili”. *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 1, Sep. 2022, pp. 330-340, doi:10.37284/jammk.5.1.853.

## UTANGULIZI

Dhana ya pragmatiki ilivumbuliwa katika miaka ya 1930 na mwanafalsafa C. W. Morris kama anavyoeleza Finch (2000). Pragmatiki ni taaluma iliyoanza kushughulikiwa kama tawi la isimu miaka ya 1970 ambapo kabla ya hapo ilihusishwa na kushughulikiwa kama tawi la falsafa, na kufafanuliwa kwa kutilia maanani misingi mikuu miwili ambayo ni: muktadha na matumizi. Katika miaka ya 1980, wataalamu walianza kuitalii pragmatiki kama maana ya msemaji na fasiri ya kile msikilizaji alichokielewa. Kwa mujibu wa Yule (1996), pragmatiki ni taaluma inayohusu uhusiano uliopo kati ya maana ya lugha na watumiaji wa mambo hayo. Ukweli kuwa utanzu huu wa isimu ni mchanga mno ukilinganishwa na tanzu zingine ni jambo ambalo limevutia watafiti wengi kuutalii ili kuukuza.

Muundo wa kirai nomino ni muhimu sana katika utafiti huu kwani kinabeba nomino ambayo ni kipengee cha kimsingi katika sintaksia na pia maneno mengi katika sentensi ya Kiswahili hutegemea nomino (Mbaabu, 1985). Kwa kawaida kirai nomino kinaweza kikatumika katika mazungumzo kupitisha ujumbe kusudiwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Katika hali kama hii, hivyo basi, kirai nomino huweza kutumika kusimba maana kimuktadha na hivyo kufanikisha ufaafu wa habari zinazokusudiwa. Maana za kimuktadha au za kipragmatiki za kirai nomino hutokana na maana za kidhahania zinazotokana na virai nomino ambazo hutumiwa katika kauli husika. Hivyo basi, maana ya kipragmatiki ya kirai nomino ni maana ya kirai nomino kimuktadha yaani kile msemaji anamaanisha japo hajakirejelea moja kwa moja.

Maana huchipuka kutokana na mpangilio wa maneno kutoka kwa msemaji hadi mpokezi wa ujumbe. Katika utafiti huu, nomino ni kipengele muhimu mno kwani hutawala maneno mengine katika sentensi na kuathiri muundo wa maneno haya katika hali yake ya utokeaji katika mpangilio wa sentensi. Utafiti huu, hivyo basi, ulilenga kutalii pragmatiki ya kirai nomino katika sintaksia ya Kiswahili ili kuongeza ujuzi uliopo kuhusiana na kirai nomino.

Makala haya yameweka bayana dhima ya kipragmatiki ya kirai nomino katika Kiswahili kwa kuongozwa na misingi ya nadharia ya Sarufi Amilifu Mfumo. Kwa mujibu wa Dale na Pearson (1978) uamilifu wa kipragmatiki humwezesha msikilizaji kuelewa maana ya neno iliyodhamiriwa, kwa kuchunguza maneno mengine katika fungu linalohusika la maneno. Maana ya neno kipragmatiki hukisiwa kutokana na namna neno hilo limetumika. Kimsingi, mbinu ya kipragmatiki inapotumika ufafanuzi wa moja kwa moja hauruhusiwi, bali msikilizaji huhitajika kurejelea mazingira ambamo neno hilo limetumika (Beck, McKeown na Kucan, 2013).

### Tatizo

Kirai nomino ni kipashio cha kimsingi katika lugha ya Kiswahili kwani hubeba kiima na shamirisho, vipashio ambavyo hukamilisha maana za kimuktadha. Hivyo basi, lazima kipengee hiki kieleweke kwa kikamilifu ili kufanikisha mawasiliano miongoni mwa wazungumzaji. Utafiti huu ulipiga hatua na kuonyesha uamilifu wa kirai nomino na hasa katika kukihusisha moja kwa moja na pragmatiki. Kirai nomino kinapotumika katika mawasiliano huonekana kumiliki nguvu fulani ya kipekee ambapo maana mbadala kando na ile ya kimsingi katika muktadha huibuka.

Hivyo basi, kirai nomino cha Kiswahili kinapotumika kimuktadha katika mawasiliano huweza kufumba ujumbe ambao humlazimu msikilizaji kuingia kwenye ulimwengu wa mzungumzaji ili aweze kubaini maana kusudiwa.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.853

Hili linapokosa kutokea, msikilizaji huishia kutopata ujumbe ambao mzungumzaji alikusudia. Jambo lingine lililozingatiwa ni kubainisha utaratibu mwafaka wa vipengele vya kirai nomino katika sintaksia ya Kiswahili.

## NADHARIA

Nadharia ya SAM hueleza jinsi lugha inavyotumika katika hali halisi ya mawasiliano. Huu huwa ni mtazamo wa kisarufi ambao husisitiza nafasi ya mawasiliano (Halliday, 1985; Halliday na Matthiessen, 2004). Jambo la kimsingi linalosisitizwa katika nadharia hii ni namna wazungumzaji huunda maana inayotarajiwa kupitia kwa matini. Nadharia ya SAM hurejelea lugha kama mfumo wa maana na uamilifu wa vipengele vinavyoihusu na kubainisha mihimili mitatu ambayo huwa ni sifa zake za kimsingi. Mihimili hiyo ni maana dhanishi, maana tagusani na maana matinishi (Eggins, 2004). Maana dhanishi imezungumziwa kwanza katika sehemu inayofuata.

### Maana Dhanishi

Maana dhanishi ni kitengo cha maana ambacho huwakilisha uwezo wa msemaji wa kutambua jambo (Halliday na Matthiessen, 1997). Kupitia maana dhanishi, tajriba za watu huwakilishwa ambazo huwa ni za ulimwengu wa kitamaduni na kijamii tunamoishi na ule wa mtu binafsi. Maana dhanishi inatuwezesha kutoa ujuzi wa ulimwengu tunamoishi na pia tajriba zetu. Maana dhanishi huwakilisha utanzu wa kisarufi wa semantiki. Semantiki ni taaluma ya isimu ambayo hufuata kanuni na taratibu maalum katika kuchunguza na kuchambua maana katika lugha. Maana hizo zaweza kuwa katika maneno, vifungu au sentensi. Pia maana zinazoshughulikiwa ni zote, ziwe za wazi au zilizofichika. Lugha hujenga mambo ya kisemantiki ambayo yanatuwezesha kufikiria kuhusu tajriba zetu. Yafuatayo ni maelezo kuhusu maana tagusani.

### Maana Tagusani

Maana tagusani huwa ni maana husishi. Inasimamia kitengo tangamanishi cha matumizi ya lugha kutegemea vikwazo vya kimawasiliano katika jamii (Halliday na Matthiessen, 1997). Kupitia maana tagusani wasemaji wanatumia lugha kwa minajili ya kuakisi, kuimarisha na kudumisha masharti ya mahusiano ya kijamii. Maana tagusani inajulikana kama amali tekelezi ya lugha ambayo huzingatia matumizi ya lugha kama tendo la usemi. Msemaji ni mtenda ambaye hujiingiza katika tendo hilo. Hivyo msemaji ni mshirika wa tendo la usemi kwa namna ambayo anajiingiza katika muktadha na hali halisi ya mawasiliano ili aweze kujieleza na kueleweka.

Msemaji anaeleweka kwa kugusia mielekeo, imani, tabia, falsafa, hisia na mawazo ya msikilizaji. Kwa upande wa kisarufi, maana tagusani inaoana na utanzu wa pragmatiki. Yule (1996) anafasili pragmatiki kama uchunguzi wa maana katika muktadha wa mazungumzo au maandishi na inavyofasiliwa na msikilizaji au msomaji. Lugha ni ishara ya kipragmatiki. Pragmatiki huangalia lugha kama mfumo wa maana kwa kutegemea muktadha wa mawasiliano. Mawasiliano yatakamilika tu pale ambapo pragmatiki itafafanua kile ambacho msemaji anaweza kumaanisha mbali na kile asemacho kwa uwazi. Muktadha unaozungumziwa katika pragmatiki ni kama vile msemaji, msikilizaji, ahali, hali, wakati na mada ya mazungumzo.

Uwasilishaji wa maana dhanishi na maana tagusani hutegemea aina ya tatu ya maana ambayo ni maana matinishi. Maelezo ya kimsingi kuhusu maana matinishi yametolewa kwa kina katika sehemu inayofuata.

## MAANA MATINISHI

Maana matinishi hurejelea jumla ya kanuni za sarufi na ufasaha wa matumizi ya lugha (Halliday na Metthiessen, 1997). Hivi ni kusema kwamba maana matinishi inaelekeza matumizi ili kumpatia msemaji vifaa vya kuwasilisha ujumbe kwa njia yenye usarifu na ufasaha kulingana na vikwazo vya muktadha na hali ya mawasiliano. Ni kupitia kwa ushirikiano wa maana dhanishi na maana tagusani ambapo maana matinishi hufanikiwa kuwakilisha ujumbe kwa namna inavyodhamiriwa.

Kwa misingi ya kisarufi tunafunganisha maana matinishi na utanzu wa sintaksia ambao unahusika na kanuni na mpangilio wa maneno katika sentensi na sheria zinazoambatana na mpangilio huo. Richards, Platt na Weber (1985) wanasema kuwa ni lazima ule mpangilio na uhusiano wa maneno kwenye sentensi au matini uwe na maana. Ukweli

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.853

huu ndio unatuwezesha kusema kwamba sintaksia hudhibitiwa na semantiki. Kwa jumla, maana matinishi huweza kuwakilisha ujumbe namna ulivyodhamiriwa kupitia kwa ushirikiano wa maana dhanishi kwa upande mmoja na maana tagusani kwa upande mwingine. Uwasilishaji na uchanganuzi wa matini unarejelea mitazamo mbalimbali ya kishazi.

## Mitazamo ya Kishazi

Matini ndogo ya kisarufi ambayo hutumiwa kama msingi wa uchanganuzi katika Sarufi Amilifu Mfumo (SAM) ni kishazi. Kishazi kimetambuliwa kuwa kipashio kidogo katika sarufi ambacho kinaweza kuchanganuliwa katika muktadha wa mawasiliano. Crystal (1985), Halliday (1985) na Radford (1997) wanazungumzia mitazamo mitatu ya kishazi ambayo ni kishazi kama uwakilishi, kishazi kama upokezano na kishazi kama ujumbe. Maelezo kuhusu kishazi kama ujumbe yametolewa kwanza.

## Kishazi kama Ujumbe

Hii ni sifa ya lugha zote. Lugha nyingi hupanga kishazi kama ujumbe kikitanguliwa na sehemu ya maudhui kisha kiarifu. Kishazi hiki huwa kina mtazamo wa kisemantiki unaolingana na maana dhanishi. Kauli hii inaweza kuwakilishwa katika Kiswahili kama inavyoonyeshwa katika *Jedwali 1*;

**Jedwali 1: Kishazi kama Ujumbe**

| Maudhui | Kiarifu |
|---|---|
| Kamau | ameenda sokoni |
| Mama | Amefika |

(Tafsiri yangu, 2022)

Kulingana na Jedwali 1 ni wazi kuwa lugha ya Kiswahili, kama zilivyo lugha nyingi, hupanga kishazi kama ujumbe ambapo nomino ‘Kamau’, na ‘mama’ zimetangulia sehemu ya kiarifu na kufuatiwa na; ‘ameenda sokoni’ na ‘amefika’ mtawaliwa, sehemu ambazo ni vijalizo vinavyotoa taarifa zaidi kuhusu ‘Kamau’ na ‘mama’. Kishazi kama ujumbe pia huwakilisha maudhui na hali katika sarufi. Kila kishazi huru huwa kinachagua hali fulani. Hali yenyewe inaweza kuwa taarifa au swali. Maswali yanaweza kuwa yenye viswahilishi au yanayotarajia majibu ya ‘ndiyo’ au ‘la,’ kwa mfano: Ulifika shuleni jana? – Jibu linatarajiwa kuwa ‘ndiyo’ au ‘la’. Maelezo kuhusu kishazi kama upokezano yametolewa katika sehemu inayofuata.

## Kishazi kama Upokezano

Kishazi kama upokezano huwa kimepangwa kama tukio la mtagusano kati ya msemaji na hadhira yake. Katika kitendo cha kuongea, msemaji hujitwika jukumu la kiusemi na katika hali hiyo anampokeza msikilizaji jukumu lake vilevile. Kwa mfano, msemaji kila anapouliza swali hutarajia jibu kutoka kwa msikilizaji, hivyo basi katika kishazi kama upokezano, msemaji anampa kitu msikilizaji au anataka kitu kutoka kwake na hivyo kupokezwa taarifa. Mambo haya yakiainishwa yanaweza kuwekwa kwa vifungu vitano vya kimsingi kulingana na uamilifu wa kiusemi ambavyo ni amri, taarifa, arifu, mshangao na shurutia (Halliday na Matthiessen, 1997). Mtazamo wa kishazi kama uwakilishi umezungumziwa katika sehemu inayofuata.

## Kishazi kama Uwakilishi

Uwakilishi wa kishazi unadhihirika kwa kubainisha ruwaza tofauti za tajriba. Kishazi ndicho kipashio ambacho kinatumika katika kuwakilisha mifanyiko au vitendo vinavyotekelezwa na akili zetu au vinavyofanyika katika ulimwengu tunamoishi. Sentensi sahili huwasilisha matendo, hisia, kuwapo kwa kitu au mtu. Haya yote yanaainishwa kwa mfumo wa kisarufi wa lugha na kuwakilishwa kupitia kishazi. Mifanyiko hii imedhihirishwa kwa kutambua mfanyiko wenye wahusika na mazingira kwenye ule mfanyiko kama inavyoonyeshwa katika *Jedwali 2*;

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.853

**Jedwali 2: Ujumbe kama Uwakilishi**

| Kirai Nomino | Kirai Tenzi | Kirai Nomino | Kirai Elezi |
|---|---|---|---|
| Mbwa | amekimbiza | Sungura | Sana |
| Mhusika | Mfanyiko | Mhusika | Mazingira |

(Tafsiri yangu, 2022)

Kutokana na *Jedwali 2* ni wazi kuwa 'mbwa' ni kirai nomino kinachowakilisha mhusika; 'amekimbizwa' ni kirai kitenzi kinachowakilisha mfanyiko; 'sungura' ni kirai nomino kinachowakilisha mhusika na 'sana' ni kirai kielezi kinachowakilisha mazingira ya hali.

Kishazi kama ujumbe kina uwiano na maana dhanishi na uteuzi wa kisarufi wa semantiki. Awali, lugha ya maana tagusani na utanzu wa pragmatiki nazo zinaoana na kishazi kama upokezano huku kishazi kama uwakilishi kikienda sambamba na maana matinishi na utanzu wa sintaksia. Mihimili ya nadharia ya SAM pamoja na mitazamo ya kishazi ilitumika katika kutekeleza lengo la makala husika.

## MBINU ZA UTAFITI

Sehemu hii ilishughulikia muundo wa utafiti, mahala pa utafiti na mbinu za kukusanya data Muundo wa utafiti ulishughulikiwa kwanza.

### Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulichukua muundo wa kimaelezo. Mbinu hii ilitumika katika utafiti huu kueleza na kutoa mifano mwafaka kuhusiana na uamilifu wa kipragmatiki wa kirai nomino. Sehemu inayofuata inaweka bayana mahala ambapo data ya utafiti ilikusanywa.

### Mahala pa Utafiti

Utafiti huu ulifanywa maktabani na nyanjani. Utafiti wa maktabani ulihusisha usomaji wa kazi mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti kama vile; vitabu, magazeti, majarida, machapisho na tasnifu mbalimbali ili kuelewa kikamilifu nadharia husika na masuala yaliyohitajika kuchanganuliwa katika matini ili kutimiza malengo ya mada ya utafiti. Kwa upande mwingine, utafiti wa nyanjani ulifanyika na ulizingatia uteuzi wa sampuli na usampulishaji pamoja na mbinu za kukusanya data. Maelezo kuhusu uteuzi wa sampuli yalitolewa kwanza.

### Mbinu za Kukusanya Data

Mbinu za ukusanyaji data zilizotumika ni hojaji na uchunzaji. Data hii ya nyanjani ilikusanywa ndani ya mazingira ya vyuo vikuu, vyuo na shule. Mbinu ya mahojiano ilizungumziwa kwanza.

#### *Mahojiano*

Mtafiti aliwahoji walimu ana kwa ana kuhusu maswali aliyoandaa ili kupata data toshelevu kuhusiana na suala la utafiti. Kila mwalimu alihojiwa kivyake baada ya kuweka miadi ya kufanya mahojiano naye. Mbinu hii ilimwezesha mtafiti kupata data pana na ya kuaminika katika utafiti huu hasa katika kuafikia lengo la pili na tatu la mada ya utafiti. Mtafiti alionelea kuwa angepata ufafanuzi zaidi kuhusu yale yaliyotekelezwa madarasani, vyumba vya maakuli, kanisani na uwanjani wakati wa uchunzaji. Walimu waliohojiwa walikuwa 35 na maswali waliyoulizwa yalimwelekeza mtafiti kuwadadisi watafitiwa kwa lengo la kupata ufafanuzi wa data zilizokusanywa kutoka, uwanjani, kanisani, vyumba vya maakuli na darasani. Mtafiti alikuwa tayari ameandaa mwongozo wa maswali ya kuongoza mahojiano. Mahojiano yaliendelezwa baada ya masomo kwa lengo la kupata ufafanuzi zaidi kuhusu mikondo iliyochukuliwa na walimu binafsi katika utekelezaji wao wa miktadha ya kipragmatiki ya kirai nomino. Iwapo maswali hayakueleweka na watafitiwa, mtafiti alichukua jukumu la kuyafafanua.

Mbinu hii vilevile huwa rahisi na haina gharama kubwa ikilinganishwa na mbinu zingine kama vile hojaji (Dooley, 1984). Mtafiti alitumia mbinu ya uchunzaji ambapo alirekodi mazungumzo halisi miongoni mwa watafitiwa kama njia ya kupata data toshelevu. Maelezo kuhusu uchunzaji yametolewa katika sehemu inayofuata.

#### Uchunzaji

Mbinu hii ilimwezesha mtafiti kutazama matukio mbalimbali katika mazingara halisi ya utokeaji

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.853

(Kothari, 2009). Uchunzaji ulifanywa ili kubainisha namna virai nomino vinavyotumika kimuktadha katika hali halisi ya mawasiliano. Ili kupata data kamilifu, mtafiti alihudhuria vipindi vya Kiswahili katika madarasa yaliyoteuliwa. Mtafiti aliketi nyuma ya madarasa na kurekodi habari zilizohitajika. Vilevile, mtafiti aliweza kurekodi habari muhimu kutoka kwa watafitiwa katika mazingira mbalimbali nyanjani kama vile kwenye vyumba vya maakuli, kanisani, uwanjani na kwenye mikutano ya vyama vya Kiswahili na kisha kuiandika data husika kwenye daftari. Data zilizokusanywa zilihusu matumizi ya kirai nomino kutegemea miktadha mbalimbali na pia changamoto za uratibu wa vipengele vya KN na hivyo, kurutubisha data iliyopatikana kupitia mahojiano.

## UAMILIFU WA KIPRAGMATIKI WA KIRAI NOMINO KATIKA SINTAKSIA

Katika sehemu hii, data zimewasilishwa kuhusu uamilifu wa kipragmatiki wa kirai nomino. Data husika zimewasilishwa kwa mujibu wa yale mtafiti aliyashuhudia nyanjani kupitia uchunzaji na mahojiano. Mtafiti alionelea kuwa ujuzi wa kiisimu wa watafitiwa ungewafanya kuwa wabunifu na wenye uelewa mpana wa matumizi ya kipragmatiki ya kirai nomino katika mawasiliano. Hivyo basi, walioshirikishwa katika kutimiza lengo husika la utafiti walikuwa ni wahadhiri kumi wa vyuo vikuu, walimu kumi kutoka vyuo wanafunzi wa vyuo vikuu, vyuo na shule za upili wote kutoka idara ya Kiswahili. Matokeo haya ni dhihirisho kuwa watafitiwa wote walikuwa na ujuzi japo mdogo wa kiisimu ambao ungechangia pakubwa katika kufanikisha lengo la utafiti.

Sehemu ifuatayo imewasilisha data kuhusu idadi ya watafitiwa waliokiri kutilia maanani uamilifu wa kipragmatiki wa KN na wale hawakutilia katika mawasiliano. Data hizi zilikusanywa kupitia mahojiano na uchunzaji na kuwakilishwa kwenye Jedwali 1 katika sehemu inayofuata.

**Jedwali 3: Utiliaji Maanani wa Uamilifu wa Kipragmatiki wa Kirai Nomino**

| Uamilifu wa kipragmatiki wa KN | Miitikio ya Wahadhiri | Asilimia (%) | Miitikio ya Walimu | Asilimia (%) | Miitikio ya Wanafunzi | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Walioutilia maanani | 4 | 40 | 7 | 28 | 20 | 31 |
| Wasioutilia maanani | 6 | 60 | 18 | 72 | 45 | 69 |
| Jumla | 10 | 100 | 25 | 100 | 65 | 100 |

Matokeo ya uchunzaji katika *Jedwali 3* yalidhihirisha kuwa wahadhiri 4, walimu 7 na wanafunzi 20 ndio walitilia maanani uamilifu wa kipragmatiki wa KN katika mawasiliano huku wahadhiri 6, walimu 18 na wanafunzi 45 wakikosa kutilia maanani uamilifu wa kipragmatiki wa KN katika mawasiliano.

Virai nomino vinapotumika katika mawasiliano huweza kuzua maana ya kipragmatiki, maana zinazochambuliwa kutokana na mfumo wa kimawasiliano. Katika kutekeleza lengo husika, uamilifu wa kipragmatiki wa virai nomino katika Kiswahili umetiliwa maanani ambapo virai nomino vimeonekana kubeba maana fiche kando na ile ya kimsingi au ya kijuujuu ambayo hujulikana kama maana ya kisemantiki.

Matokeo ya uchunzaji kuhusu uamilifu wa kipragmatiki wa KN yalidhihirisha kuwa wahadhiri 5, walimu 8 na wanafunzi 5 waliweza kutumia virai nomino ambavyo vilifumba maana ya kipragmatiki. Walimu 3 miongoni mwa wale waliotumia virai nomino vilivyofumba maana kimuktadha, waliwaelekeza wanafunzi kusoma taarifa na kufafanua virai nomino vilivyodokezwa kwenye ufahamu. Ufafanuzi huu ulitilia maanani uelekezi unaotolewa na Tomlinson na Ellis (1992) kuwa ufafanuzi wa vipengele vya kileksia unafaa kutilia maanani hatua nne ambazo ni kufafanua, kubainisha matumizi halisi kupima ufahamu wa wanafunzi na kumpa fursa ya kufanya mazoezi.

Wahadhiri 5 waliwashirikisha wanafunzi katika kujadili maana ya kipragmatiki za baadhi ya virai nomino walivyovitumia katika mihadhara huku wakiwakosoa hapa na pale. Wanafunzi 5 walitumia virai nomino vilivyofumba maana za kimuktadha kwa ama kuwarejelea wenzao au kuzungumzia masuala yanayowazunguka. *Jedwali 4* katika

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.853

sehemu inayofuata limewasilisha matokeo yaliyopatikana wakati wa uchunzaji.

**Jedwali 4: Idadi ya Virai Nomino Vilivyofumba Maana ya Kipragmatiki**

| Watafitiwa | Idadi | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Wahadhiri | 5 | 28 |
| Walimu | 8 | 44 |
| Wanafunzi | 5 | 28 |
| Jumla | 18 | 100 |

Katika *Jedwali 4*, inadhihirika kuwa wahadhiri na wanafunzi walitumia idadi sawa ya virai nomino huku walimu wakitumia virai nomino vinane katika miktadha mbalimbali ya kimawasiliano. Jedwali 3 katika sehemu inayofuata limewakilisha baadhi ya virai nomino vilivyodondolewa kutokana na kauli zilizotumiwa na watafitiwa katika mawasiliano yao. Virai nomino hivi vilidhihirisha kufumba maana ya kipragmatiki. Data hizi zilitokana na wahadhiri, walimu na wanafunzi.

**Jedwali 5:Virai Nomino Vilivyofumba Maana ya Kipragmatiki**

| Virai Nomino |
|---|
| Chege anaienzi **nyumba yake** |
| Mtu mzee ni **dawa** |
| Mwangi amepata **mtoto** |
| Mwalimu alimpa **miti** baada ya kufeli mtihani |
| Wanjiku amenunua Mercedes-Benz mpya |
| Esther aliolewa na **mwanamume** |
| Baba, yeye ni **mtu mzima** |
| Baba, yeye ni **mtoto** |
| Mwalimu analipenda **darasa lake** |
| Kibe amepewa **bendera** |
| Maonyesho ya leo yatakuwa **motomoto** |

Katika *Jedwali 5*, vifungu vyote kuanzia 1-11; ambavyo vimeandikwa kwa kukolezwa rangi ni virai nomino ambavyo vimefumba maana ya kipragmatiki. Hivyo basi, uamilifu wa kipragmatiki wa kirai nomino katika Kiswahili sanifu umeelezwa kupitia vielelezo sentensi (Taz. Jedwali 5) ambazo zimesheheni virai nomino vilivyotumika kurejelea miktadha mbalimbali ya kijamii na kudhihirisha kufumba maana za kipragmatiki. Uwezo huu wa virai nomino kupata maana mpya kimuktadha unaweza kuelezwa kwa kutumia nadharia ya SAM ambapo jumbe zinazotolewa zina ufaafu kwa msikilizaji, pamoja na uwezo wa mpokezi kuzisimbua ni uwezo wa kimawasiliano ambao hutenda kazi katika mazungumzo halisi. Vilevile, virai nomino vimetumika kimuktadha na wazungumzaji kwa kusudi la kuhusishwa katika mawasiliano na kuelekezwa kwenye ujumbe muhimu ulio katika mazungumzo hayo. Kwa mujibu wa Ullman (1970), mbinu inayotumika na wazungumzaji wa virai nomino husika ni ile ya upanuzi wa maana ambapo maana nyingine za kipragmatki huibuka katika miktadha mipya.

Kwa mujibu wa Corder, Perrin na Smith (1968) maneno yanaweza kugawanywa katika makundi matatu. Kundi la kwanza ni la maneno yanayorejelea vitu halisi. Kundi la pili ni maneno yanayorejelea sifa za kiuhusiano. Maneno hayo ni ya kiuhusiano kwa sababu hufafanuliwa kutegemea hali inayohusishwa na vitu vyenyewe. Kwa mfano katika kipindi kimoja mwalimu mmoja alitoa kauli *Chege anaienzi nyumba yake* na kuwauliza wanafunzi kutoa maana ya kirai nomino *nyumba yake*.

Kwa mujibu wa majibu 9 yaliyotolewa na wanafunzi, kirai nomino *nyumba yake* kiusemi kina maana ya *jengo anamoishi Chege. Hata hivyo*,

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.853

katika ufafanuzi wake, mwalimu huyo alieleza kuwa KN hicho kinaweza kutolewa fafanuzi tofauti kutegemea jamii husika, mathalan, katika jamii moja kirai nomino hicho kinaweza kumaanisha *familia yake* na kirai nomino *nyumba yake* kinafumba maana ya kipekee kinapotumika katika mazungumzo. Ufasili huu unalingana na maelezo ya Halliday na Matthiessen, 1997) ambayo yanadokeza kuwa kupitia maana tagusani wasemaji hutumia lugha kwa minajili ya kuakisi, kuimarisha na kudumisha masharti ya mahusiano ya kijamii.

Kundi la tatu la maneno kwa mujibu wa Corder, Perrin na Smith (1968) ni lile linalorejelea vitu dhahania au dhana za kijumla. Wanaeleza kuwa kwa vile maneno mengi katika kundi hili hurejelea dhana pana jambo ambalo husababisha utata katika kuyatumia. Hili lilidhihirika katika kipindi kimoja wakati mhadhiri alizua mjadala kuhusu maana ya kirai nomino *dawa* katika sentensi *mtu mzee ni dawa*. Baadhi ya maana zilizotolewa na wanafunzi ni *tiba, kago, majuni*, na *hirizi*. Japo mwalimu alieleza kuwa maana zote zilizotolewa na wanafunzi zilikuwa sawa, alifafanua kuwa kirai nomino *dawa* kiliweza kufumba maana ya *wosia* unaotolewa na mtu mzee. Ufafanuzi huu unalingana na maelezo ya Halliday na Matthiessen (1997) kuhusu maana dhanishi. Wanaeleza kuwa kupitia maana dhanishi, maana zote hushughulikiwa, yaani zilizo wazi na zilizofichika kwa kutilia maanani tajriba za ulimwengu halisi wa kitamaduni, kijamii na ule wa mtu binafsi. Hivyo basi, kirai nomino *dawa* kilifumba maana kipragmatiki ya *wosia*, unaofananishwa na *dawa* iliyo na uwezo wa kutibu ujinga na upumbavu unaohusishwa na maisha ya ujana.

Aidha, maneno mengi hutumiwa na watu tofauti kumaanisha mambo tofauti. Hali hii husababisha baadhi ya maneno kuhusishwa na maana mpya, ambazo awali hazikuhusishwa na maneno hayo. Kwa mfano katika kipindi kimoja mhadhiri mmoja aliuliza wanafunzi wake kutoa maana ya kirai nomino *mtoto* katika sentensi *Mwangi amepata mtoto*. Baadhi ya maana zilizotolewa ni *mwanadamu aliye na umri mdogo*, *kitu kidogo* na *kiumbe kinachozaliwa na mwanadamu*. Mhadhiri aliwaeleza kuwa japo maana hizo zingekubalika katika miktadha fulani, maana iliyotolewa haikuwa iliyokusudiwa katika muktadha wa sentensi husika. Baadaye mhadhiri alifafanua kuwa kirai nomino *mtoto* kilitumika kimuktadha kumaanisha kuwa *Mwangi* amepata *mchumba*. Ufafanuzi huu unalingana na maelezo ya Yule (1996) kuhusu pragmatiki, anaeleza pragmatiki kama uchunguzi wa maana kutegemea muktadha wa mawasiliano na unavyofasiliwa na msikilizaji. Vilevile, kauli Chege amepata mtoto, inalingana na maelezo ya Halliday na Matthiessen (1997) kuhusu kishazi kama ujumbe. Kauli hapo juu imewasilisha kishazi kama upokezano kwani kimepangwa kama tukio la mtagusano kati ya msemaji na hadhira yake kwani inaonyesha kifungu chenye uamilifu wa kiusemi ambao ni kutoa taarifa.

*Mwalimu alimpa miti baada ya kufeli mtihani* ni mojawapo ya data iliyotokana na uchunzaji ulifanywa kwenye chumba cha mamkuli. Maana ya juu juu ya kauli hiyo ni tata. Kirai nomino kinachotiliwa mkazo katika kauli hapo juu ni *miti*. Kimsingi, kina maana kuwa mwanafunzi anayezungumziwa alipewa miti, yaani mimea. Hata hivyo, kutegemea muktadha wa kimazungumzo, maana hii haikubaliani na ujumbe ambao mtoa kauli alidhamiria kupitisha.

Kwa mujibu wa Halliday na Metthiessen (1997), mfasili wa kirai nomino *miti*, hana budi kufahamu na kujiingiza kwenye ulimwengu wa kimawazo wa mtoa kauli husika ili aweze kubaini kile anachomaanisha kando na kile asemacho kwa uwazi. Hivyo basi, katika muktadha wa kiusemi, kirai nomino *miti* kinamaanisha kuwa anayezungumziwa *alichapwa viboko* na mwalimu wake baada ya kufeli mtihani.

Kauli nyingine iliyotokana na watafitiwa ilikuwa ni “Maonyesho ya leo yatakuwa motomoto”. Mojawapo wa mambo yanayozingatiwa na maana tagusani ni hali, jambo ambalo linajitokeza wazi katika sentensi (Halliday na Matthiessen, 1997). Hivyo basi, maana ya kimuktadha inayowasilishwa na kirai nomino *motomoto* ni kuwa maonyesho ya siku hiyo yangependeza, kufurahisha na hata kuvutia. Aidha, ili kuelewa ujumbe katika kirai nomino *motomoto*, mfasili hana budi kutumia ujuzi wa maana tagusani maana ambayo huona na utanzu wa pragmatiki, ili kufafanua kile msemaji anamaanisha mbali na kile asemacho kwa uwazi Halliday na Matthiessen, (1997). Fafanuzi za kirai nomino miti na motomoto hapo juu, zinalingana na

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.853

maelezo ya Sperber na Wilson (1986) yanayofafanua kuwa, ili mpokezi wa kauli hapo juu aelewe kile mzungumzaji anamaanisha, hana budi kutumia ufahamu wa utamaduni pamoja na muktadha ambapo maana ya virai nomino *miti* na *motomoto* vinahamishwa na kupewa maana nyingine katika muktadha wa mazungumzo.

Kwa mujibu wa Sperber na Wilson (1986), mzungumzaji hutumia maana iliyo wazi huku msikilizaji akihitajika kutambua maana ya kile alichokusudia mzungumzaji na kuisimbua maana kwa kutumia muktadha, urejelezi na ufaafu wa ujumbe ambao utamwezesha msikilizaji kupata maana iliyokusudiwa japo haikubainika kiusemi. Hili lilidhihirika katika kipindi kimoja wakati mhadhiri alizua mjadala kuhusu maana ya virai nomino *Mercedes-Benz mpya* katika sentensi Wanjiku alinunua *Mercedes- Benz mpya* na *mwanamume* katika sentensi *Esther ameolewa na mwanamume*.

Mojawapo ya jibu lililotolewa na wanafunzi kuhusu kirai nomino *Mercedes- Benz mpya* ni kuwa ni *aina ya gari*. Hata hivyo, mhadhiri alifafanua na kueleza kuwa KN *Mercedes-Benz mpya* kilifumba maana ya *gari la kifahari* na wala sio gari tu kama walivyodhani wanafunzi wengi. Kwa upande mwingine wanafunzi walieleza kuwa kirai nomino *mwanamume* kilimaanisha kuwa Esther amepata *bwana*, *msaidizi*, *msiri*, *amefunga pingu za maisha* au *ameoleka*. Mhadhiri alitoa ufafanuzi kuwa, japo majibu yaliyotolewa na wanafunzi yalikuwa kweli kwa kutegemea miktadha mbalimbali, hayakulingana na muktadha wa kauli aliyoitoa.

Kimuktadha, maana ya kirai nomino mwanamume ni kuwa, Esther ameolewa na mwanamume wa kipigiwa mfano anayemtunza; yaani anayefahamu majukumu yake kwa mkewe kinyume na ilivyo na wanaume wengine ambao katu hawatekelezi majukumu yao ipasavyo kwa wakeo. Fafanuzi hizi za kipragmatiki za virai nomino Mercedes- Benz mpya na mwanamume zinalingana na maelezo ya Yule (1996) kuhusu ufasiri wa maana za kipragmatiki ambayo yanadai kuwa ili mpokezi wa kauli aweze kufasiri kauli husika kwa usahihi, hana budi kufahamu taratibu na mbinu za kiufahamu za awali, zitakazomwezesha kuzichanganua kauli hizo kutokana na uwezo wa kuelewa utamaduni na ulimwengu mnamotumika dhana hizo.

Kwa mujibu wa Sperber na Wilson (1986), fasili ya kauli humfikia mpokezi kwa kuhusisha fahamu za awali na muktadha ili kupata maana iliyokusudiwa. Hili lilidhihirika katika kipindi kimoja wakati mwalimu mmoja alipowauliza wanafunzi kueleza maana ya kirai nomino *mtu mzima* katika sentensi *Baba, yeye* ni mtu mzima na *mtoto* katika sentensi *Baba, yeye ni mtoto* kama ilivyojitokeza katika mojawapo ya mchezo wa kuigiza. Mwanafunzi mmoja alifafanua kuwa analomaanisha mzungumzaji kupitia kirai nomino *mtu mzima* ni kuwa *anayemrejelea ana uwezo wa kufanya uamuzi kivyake kuhusiana na mambo yake kwani anajua yaliyo na manufaa kwake na ambayo yanaweza kumdhuru maishani*. Mwanafunzi mwingine aliongeza na kusema kuwa kirai nomino *mtu mzima* kina maana kuwa *anayezungumziwa apewe uhuru wa kujiamulia masuala yake na kwa mtazamo wake, anayerejelewa ana umri unaomruhusu kufanya uamuzi wa mambo muhimu maishani mwake*.

Kwa upande mwingine, katika sentensi ya pili, mwanafunzi mmoja alidai kuwa alichomaanisha mzungumzaji ni kuwa, anayerejelewa ana umri mdogo na hivyo sio vyema kuachwa kufanya uamuzi kuyahusu masuala muhimu maishani mwake kwani huenda akafanya maamuzi ambayo kamwe hayawezi kumfaa na hata kwa wakati yakamletea masaibu maishani mwake kwani umri wake haumruhusu kujifanyia maamuzi. Fafanuzi hizi zinalingana na maelezo ya Halliday na Matthiessen (1997) kuhusu maana tagusani ambayo hueleza kuwa msemaji hutoa kauli ambazo anatarajia msikilizaji wazo ataweza kung'amua ujumbe anaokusudia kuupitisha. Hivyo basi, msikilizaji wake huweza kuufasiri ujumbe uliopo bila kupotosha maana kusudiwa ambayo kwa kawaida huwa ni ya kipekee.

Kwa mujibu wa Thomas (1995), muktadha unapobadilika, maana ya neno pia hubadilika. Hili linadhihirika kupitia kauli mbili, ya kwanza ikiwa, "*Mwalimu analipenda darasa lake*" iliyotolewa na mwalimu mmoja akimrejelea mwenzake. Pili, *Kibe amepewa bendera*. Katika kauli ya kwanza hapo juu kirai nomino cha yambwa ni *darasa lake* ambacho kina muundo wa nomino *darasa* na kivumishi kimilikishi ambacho ni *lake*. Maana msingi ya kirai nomino *darasa lake* ni kuwa ni *jengo ambamo wanafunzi hupokea mafunzo* lakini katika kirai nomino *darasa lake* maana ya kidhahania

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.853

inayowasilishwa ni kuwa *mwalimu anawapenda wanafunzi wake*.

Kauli ya pili, "*Kibe amepewa bendera"* ina virai nomino viwili, cha kwanza kikiwa ni *Kibe* na cha pili ni *bendera*. Kirai nomino cha pili 'bendera' kinapata maana ya kipekee kando na ile maana msingi. Maana ya kipragmatiki ya kirai nomino 'bendera' ni uongozi, ikiwa na maana kuwa anayerejelewa katika sentensi husika, ambaye ni Kibe, amepata uongozi au madaraka katika mahala pake pa kazi.

## HITIMISHO

Matokeo ya data ya uchunzaji yamedhihirisha kuwa katika uamilifu wa kipragmatiki wa KN, mzungumzaji hutoa ujumbe ambao maana yake ni fiche na msikilizaji hulazimika kuchambua kile mzungumzaji ananuia kuwasilisha kwa kutilia maanani muktadha wa mazungumzo. Hivyo basi, msikilizaji hana budi kufahamu utamaduni na kaida za mawasiliano za ulimwengu wa mzungumzaji ili aweze kufasiri taarifa husika bila kupotosha maana ya kile mzungumzaji alikusudia kwa kuzingatia muktadha wa mazungumzo.

Matokeo haya vilevile yamelingana na maelezo ya Habwe na Karanja (2004) kuhusu maana msingi ya neno ambayo kwa kawaida huwa haibadiliki kutokana na athari za kipragmatiki. Aidha, maana zingine zinazoibuka kutokana na maana msingi hutokana na maana ya msemaji kwa kutilia maanani muktadha wa kimawasiliano.

## MAREJELEO


Beck, I. L., McKeown, M. G., & Kucan, L. (2013). *Bringing words to life: Robust vocabulary instruction*. Guilford Press.

Corder, J. W., Perrin, G. P., & Smith, G. H. (1968). *A Handbook of Current English.* 3rd ed. Illinois, Scott, Foresman & Company.

Crystal, D. (1985). *A Dictionary of Linguistic and Phonetics*. Oxford: Basil Blackwell Limited.

Dale, D. J., & Pearson, P. D. (1978). *Teaching Reading Vocabulary*. New York, Holt, Richard & Winston.

Dooley, D. (1984). *Social Research Methods.* New Jersey: Prentice Hall inc.

Eggins, S. (2004). *An introduction to systemic functional linguistics* (2nd ed.). London: Bloomsbury Academic.

Ellis, R. (1992). Learning to communicate in the classroom: A study of two language learners' requests. Studies in Second Language Acquisition, 14, 1-23.

Finch, G. (2000). *Linguistic Terms and Concepts*. New York. Palgrave Macmillan.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Halliday, M. & Matthiessen, C. (1997). *Construing experience through meaning: alanguage-based approach to cognition*. Berlin and New York, Walter de Gruyter.

Halliday, M., & Matthiessen, C. (2004). *An Introduction to Functional Grammar* (2nd ed.). London: Arnold.

Halliday, M. A. K. (1985). *An introduction to functional grammar*, London: Edward Arnold.

Kothari, C.R. (2009). *Research Methodology. Methods and Techniques* (Toleo la pili), New Delhi; New Age International (P) Limited Publishers.

Matthiessen, C., & Halliday, M. (1997). *Systemic functional grammar* (1st ed.).

Mbaabu, I. (1985). *Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Kenya Publishing and Book Marketing Co. Ltd.

Radford, A. (1997). *Transformational Grammar*. Great Britain: Cambridge University Press.

Richards, J., C. Platt, J., & Weber, H. (1985). *Longman Dictionary of Applied Linguistics.* London: Longman.

Sperber, D., & Wilson, D. (1986). *Relevance, Communication and Cognition.* Oxford: Blackwell.


This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.853

Thomas, J. (1995). *Meaning in Interaction*. Edinburg: Pearson Education.

Tomlinson & Ellis, R. (1992). Learning to communicate in the classroom: A study of two language learners' requests. *Studies in Second Language Acquisition*, *14*, 1-23

Ullman, S. (1970). Semantics: An Introduction to the Science of Meaning. Oxford: Basil Blackwell.

Yule, G. (1996). *Pragmatics*. New York: Oxford University Press.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.